# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230
Tovuti: [www.zanzibarassembly.go.tz](http://www.zanzibarassembly.go.tz)

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: [zahore@zanlink.com](mailto:zahore@zanlink.com)

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILINO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.

***Mheshimiwa Spika,*** leo hii Kamati yangu inawasilisha Ripoti yake ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kwa msingi huo, nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa kujadili Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza lako tukufu.

***Mheshimiwa Spika,*** ni dhahiri kuwa weledi, busara na uwezo mkubwa unaouonesha katika kuliongoza Baraza hili, pamoja na wasaidizi wako umekuwa chachu ya mafanikio ya chombo hiki.

***Mheshimiwa Spika***, pia napenda kutoa shukurani kwa Wizara zote ambazo zipo chini ya Kamati yangu kwa ushirikiano wao wanaotupatia kupitia kazi zetu za Kamati katika kipindi chote hiki na kuweza kufanikisha hadi leo kutoa ripoti mbele ya Baraza lako Tukufu.

***Mheshimiwa Spika***, Kadhalika nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kuendelea kuniamini na kunipa imani ya kuwaongoza na kutoa mashirikiano makubwa, jambo ambalo linaendelea kunipa nguvu na pia limesaidia kufanikisha vizuri majukumu ya Kamati yetu. Kwa hakika ustahamilivu, weledi na umahiri wao umesaidia kwa kiasi kikubwa sana kupatikana hadi kuwasilishwa kwa ripoti hii.

***Mheshimiwa Spika,*** nakuhakikishia kwamba Wajumbe wangu wamefanya kazi nzuri katika kuhakikisha Kamati inaisimamia vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba yetu na maslahi ya Taifa zima. Na hapa napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe Yahya Rashid Abdullah | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe Hudhaima Mbaraka Tahir | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 5. | Mhe Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| 6. | Mhe Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| 8. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

***Mheshimiwa Spika***, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 107 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 na majukumu yake ni kama yale yaliyoelezwa katika jadweli la Kwanza. Kamati hii inafanyakazi na Wizara tatu zifuatazo: -

(1) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

(2) Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

(3) Wizara ya Maji, Nishati na Madini

## 1) WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati, inaunga mkono juhudi za Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa jitihada zake kutaka kuifungua Pemba kiuchumi na

kuifanya kuwa kituo mahsusi cha uwekezaji kwa uimarishaji wa miundombinu ya Barabara, Bandari na Uwanja wa Ndege.
Katika kuunga mkono suala hilo kwa makusudi kabisa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilijipangia kwenda Pemba kwa kila mzunguko wa kazi ili kukagua na kufuatilia kwa karibu na kuhamasisha azma hiyo ya serikali.

## MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yangu imepokea taarifa na kufanya ziara katika maeneo ya miradi ya Maendeleo ya Wizara ili kujiridhisha, lakini kinyume na matarajio ya Kamati, miradi mingi tumebaini inasuasua huku ikukumbwa na changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa fedha na tatizo la fidia kama ilivyofafanuliwa katika Ripoti ya Kamati.

### Ujenzi wa Barabara ya Wete - Chake kilomita 22.1.

***Mheshimiwa* Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu Nne Unguja na Pemba ikiwemo Barabara ya Wete – Chake kilomita 22.1 ni miongoni mwa miradi iliyoguswa katika ripoti ya Kamati yetu. Hadi tunatayarisha ripoti hii ujenzi huu umegubikwa na changamoto kubwa ya Fidia na ulikuwa umefikia asilimia **8.8%** ya utekelezaji. Kamati yangu inaishauri Serikali kupitia Wizara kuwa na utaratibu mzuri utakaohakikisha wananchi wanaoathirika na rasilimali zao kwa kupisha miradi ya Maendeleo wanapata fidia kwa wakati na thamani halisi kulingana na wakati na mfumko wa bei.

### Mradi wa Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba

***Mheshimiwa Spika,*** Miongoni mwa hatua za Serikali za kuifungua Pemba kiuchumi ni Uimarishaji wa uwanja wa ndege wa Pemba ili ukidhi mahitaji ya ongezezeko la abiria na wakati wa sasa kwa kuazimia kuutanua uwanja huo pamoja na jengo jipya la kusubiria abiria. Ufuatiliaji wa Kamati umebaini, hatua za ujenzi zitaanza baada ya kukamilika hatua za "Mobilization" kwa mjenzi huyo na Serikali kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yataathiriwa na ujenzi huo. Kamati inaitakia kheri Wizara na Serikali kwa ujumla kwa habari hizi njema na zinazolenga kuongeza

safari za mashirika ya ndege na pia kukuza mapato ya taifa.

***Mheshimiwa Spika,*** Wakati Wizara ikisubiri kuanza kwa mradi huo mkubwa, Kamati inashauri kufanyiwa kazi changamoto zote zilizoainishwa kwenye Ripoti ya Kamati ikiwemo kuongeza Mashine za ukaguzi  wa mizigo (X-RAY MACHINE) Pamoja na kuimarisha ofisi za ziliopo Uwanjani hapo  ili ziweze kufanya majukumu yao  kwa ufanisi mzuri kulingana na wakati wa sasa.

**Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)**

***Mheshimiwa Spika,*** katika Ripoti yetu, Pia tumeangalia uimarishaji wa miundombinu ya Bandari hasa Bandari ya Mkoani pamoja na Bandari mama ya Malindi. Kamati ilitembelea Bandari ya Malindi na kushuhudia Shughuli za uchimbaji kuzidisha kina cha maji ili kuongeza eneo jengine la kuegeshea meli ili kukabili changamoto ya udogo wa gati sambamba na Ujenzi wa eneo la kuwekea makontena Bwawani ili kuondosha tatizo la Ufinyu wa eneo la kuhifadhia makontena.

***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hali hiyo ya matumaini, udadisi wa Kamati umebaini kwamba,  katika kuimarisha  huduma za Bandari ya Malindi Serikali imejipanga kutafuta muendeshaji wa Bandari ili kuongeza ufanisi. Katika utekelezaji wa jambo hili, Kamati inaiomba Wizara ihakikishe hatma njema kwa wafanyakazi wa Bandari ya Malindi baada ya kukabidhiwa kwa mwekezaji.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yangu imefarajika baada ya kushuhudia kazi za kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa ajili ya kuhudumia meli za Makontena, uhifadhi wa makontena, pamoja na Kujenga upya njia ya watembea kwa miguu. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri kuangaliwa vyema suala la kituo cha mafuta kilichopo karibu na eneo la kuhifadhia makontena pamoja na kituo cha Daladala mbele ya Mlango Mkuu wa Bandari ya Mkoani  ambacho kinaweza kuleta ufumbufu wakati  wakati badnari ya mkoani itakapokamilika kwanu tunaamini kutakuwa na harakati nyingi za kutoka na kuingia bandarini hapo.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia inashauri Shirika la Bandari kuendelea kusimamia na kuendeleza mipango yake ya Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani, uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni na Shumba Bandari ili kuipunguzia mzogo wa msongomano wa abiria na mizigo katika bandari kuu ya Malindi.

**Wakala wa Barabara Zanzibar**

***Mheshimiwa Spika,*** Programu ya Usafirishaji Utekelezaji wake unaendelea kuwa ni changamoto, kama inavyobainishwa katika Ripoti yetu. Tukisoma eneo la Wakala wa Barabara tutabaini kwamba nae kwa asilimia kubwa ameshindwa kufanya takriban shughuli zote alizojipangia kutokana na ukosefu wa fedha kutoka serikalini. Ripoti yetu imezibainisha Shughuli ambazo Wakala wa Barabara ameshindwa kuzifanya ikiwa ni pamoja na: -

1. Kushindwa Kujenga barabara mbalimbali Unguja na Pemba zikiwemo barabara za Unguja Ukuu – Uzi Ngambwa, Tumbatu, Kiboje - Ukuchuni, Micheweni-Msasani na Kijangwani – Birikau.
2. Kushindwa Kufanya Matengenezo mbalimbali ya barabara Unguja na Pemba ikiwemo Chanjamjawiri – Tundauwa, Chanjani – Pujini,Mizingani – Wambaa na Kenya- Chambani
3. Kushindwa Kujenga misingi 26 ya maji ya mvua
4. Kushindwa Ujenzi wa Madaraja na Makalvati Unguja na Pemba ikiwemi Machui, Chamanangwe na Vitongoji
5. Kushindwa kufanya Kazi za utunzaji wa Barabara Unguja na Pemba katika barabara nyingi za Unguja na Pemba.
6. Kushindwa Kuweka Miundombinu ya usalama barabarani katika baadhi ya barabara.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawapatia fedha za kutosha na kwa wakati Wakala wa Barabara ili aweza kutekeleza majukumu yake kwa muda uliopangwa. Lakini pia ni busara kuangaliwa malengo yatayoweza kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha na kuacha utaratibu wa kujipangia malengo mengi

ambayo mwisho wa siku Wizara inashindwa kuyakamilisha.

**Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani.**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mara nyengine tena Kamati inahimiza kuchukuliwa hatua za uwekaji wa alama za Barabarani kwa Unguja na Pemba ili kuepusha ajali zitokanazo na ukosefu wa uwepo wa alama yoyote inayoashiria tahadhari kwa watumiaji wa barabara, kwani imekua ni changamoto ya muda mrefu tena kwa barabara kongwe na mpya kukosa alama hizo lakini pia, Kamati inasisitiza kuzibwa mashimo yaliyopo katika barabara zetu mara tu yanapoanza ili kuondosha usumbufu na kupunguza ajali zitokanazo na uwepo wa mashimo hayo kwa barabara zetu nyingi mjini na vijijini.

***Mheshimiwa Spika,*** Miongoni mwa mbinu zilizotumiwa na Kamati yangu katika kukusanya taarifa za Ripoti yetu ni kuzungumza na wadau. Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wadau wa masuala ya Usafiri wa Barabarani na Bandari ambao kwa pamoja walilalamikia suala la gari zinazotoke nje ya Zanzibar zikiwa tayari na mizigo na kuisambaza katika maeneo yote ya Zanzibar, shughuli ambayo wanadhani ikiweza kufanywa na gari na madereva walipo hapa Zanzibar ambao wanalipa vibali vyote vinavyohusiana leseni na ruhusa ya njia.

***Mheshimiwa Spika*,** hapa tunaiomba Mamlaka iwe na utaratibu unaofahamika wa vibali vya njia na matumizi ya Barabara kwa gari zote zinazotokea nje Zanzibar zikiwa tayari na mizigo na kuisambaza katika maeneo yote ya Zanzibar.

***Mheshimiwa Spika*,** Hoja nyengine iliyoibuliwa na wadau wa Usalama barabarani ni muhali wa kuwachukulia hatua baadhi ya madereva wanaokiuka miongozo, kanuni na sheria za usalama barabarani jambo ambalo linachangia makosa na ajali za barabarani na baadae kusababisha ajali zinazoendelea kupoteza nguvu kazi ya taifa.

**Shirika la Meli**

***Mheshimiwa Spika,*** Katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Ripoti yetu inamalizia na Shirika la Meli Zanzibar, ambalo limeuza meli mbili (2) ambazo ni MV

Maendeleo na MT. Ukombozi lakini limeshindwa kuiuza Meli yake ya MV Mapinduzi II kutokana na wazabuni kutofikia bei elekezi iliyowekwa na mtathmini Mkuu wa Serikali. Tunaiomba Serikali kutafuta njia sahihi na mbadala matumizi ya Meli ya MV Mapinduzi II ili iweze kuleta tija kwa Shirika na Taifa kwa ujumla badala ya kuendelea kuleta hasara.

## WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu pia imechambua muundo, programu na utekelezaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ambayo inadhamana ya kuhakikisha wananchi wanapata makaazi bora, yaliyosalama na nafuu.

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara**

***Mheshimiwa Spika,*** **Kamati** yangu inaendelea kusisitiza kufanyiwa marekebisha Sheria zote ambazo zimeshapitwa na wakati na utekelezaji wake hauendani na hali halisi ya sasa ikiwemo Sheria ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Sheria ya Mahkama ya Ardhi na Sheria ya Mipango Miji na Vijiji ili kuweza kuondosha changamoto iliyopo hivi sasa za utekelezaji wake.

**Aidha,** Kamati inaendelea kuihimiza Wizara kufanya jitihada za makusudi za kutatua changamoto ya uhaba wa wafanyakazi wa fani za kitaalamu ambao bado kuna upungufu mkubwa katika taasisi zake nyingi ili kuweza kuisaidia Wizara katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilikutana na watendaji wa Afisi Kuu Pemba, Afisi yenya jukumu la kuratibu na kusimamia utawala na mipango ya kazi za Wizara zinazotekelezwa Pemba na kubaini Ufinyu wa bajeti na upungufu mkubwa wa wafanyakazi wataalamu katika sekta zote za Wizara hii. Aidha Kamati imekuta Upungufu wa vitendea kazi, pamoja na Uchakavu wa baadhi ya nyumba za Serikali. Kamati inazidi kujenga matumaini kwamba, wizara itaongeza bajeti kwa Ofisi Kuu Pemba ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi pamoja na kununua vitendea kazi kama vile vifaa vya upinaji na magari.

**Programu Kuu ya Usimamizi wa Ardhi na Makaazi**

***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa changamoto kubwa ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ni migogoro ya ardhi, Kamati inadhani katika kupambana na changamoto hiyo ni kuziimarisha kiutendaji taasisi zetu zinazosimamia Masuala ya ardhi ikiwemo Kamisheni ya Ardhi pamoja na Mahakama ya Ardhi ambazo zinakabiliwa na tatizo la vifaa, ufinyu wa bajeti, uchakavu na udogo wa majengo ya ofisi na watenda kazi.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati iletembelea Afisi ya Kamisheni ya Ardhi Pemba na kushtushwa na hali mbaya na hatarishi ya jengo wanalotumia hivi sasa. Kamati ilishuhudia jengo hilo likiwa limezungukwa na nyufa huku likitishia usalama wa watendaji na nyaraka zilizomo. Lakini pia, kwa jengo lao liliopo Unguja nalo lipo katika hali mbaya na isiyoridhisha kwani jengo ni chakavu na linavuja. Kamati inaishauri Wizara kuihamisha Kamisheni katika jengo hilo liliopo Macho Mane, pamoja na kuangalia hatua zinazofaa kuchukuliwa kwa jengo lao liliopo Unguja.

***Mheshimiwa Spika*****,** Ripoti yetu pia imegusia masuala ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambayo ni dhamana katika kazi za uthamini kwa Serikali, Sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Ofisi hii, kama zilivyo taasisi nyengine za Wizara hii, nayo inakabiliwa na tatizo la ufinyu wa Bajeti, vitendea kazi na wataalamu.

Aidha Kamati inashangazwa na muundo wa afisi hii ambayo haina mfanyakazi hata mmoja huko Pemba. Ripoti yetu inatowa mapendekezo kadhaa ambayo tunaamini yakitekelezwa yanaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha utendaji wa afisi hii.

**Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA)**

***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Majengo ina wajibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo. Katika nyakati tafauti Kamati yetu imekuwa ikikutana na watendaji wa taasisi hiyo na kubaini nayo imekabiliwa na changamoto nyingi zinazorejesha nyuma utendaji. Changamoto hizo ni pamoja na:-

a) Ukosefu wa fedha za kutekelezea majukumu waliojipangia

b) Ukosefu wa Ofisi ya kudumu.
c) Upungufu wa vitendea kazi pamoja na teknolojia za kisasa.
d) Baadhi ya Miradi ya Serikali bado haipitii kwa Wakala wa Serikali
e) Kuwepo na uelewa mdogo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali juu ya majukumu ya Wakala wa Majengo katika usiamamizi wa nyumba za Serikali.

***Mheshimiwa Spika***, Kamati inaendelea kushauri kwa mara nyengine tena kuchukuliwa hatua za haraka kuhakikisha kuwepo na utaratibu mzuri wa uingizwaji wa fedha zinazopangwa ili waweze kuzitumia kwa kukamilisha malengo yao ikiwemo la kukarabati nyumba za Serikali ambazo nyingi ni chakavu. Pia, Kamati inatoa wito kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo katika miradi yao ili waweze kutoa ushauri wa kitaalamu na kuweza kusaidia kufanikiwa kwa miradi hiyo na kuwa na ubora unaotakiwa.

**Shirika la Nyumba Zanzibar**

***Mheshimiwa Spika,*** kwa Upande wa Shirika la Nyumba, Kamati yangu imebaini kuendelea kwa tatizo la madeni makubwa na ya muda mrefu kwa wapangaji wa shirika jambo ambalo linasababisha kukosa fedha za kuziendeleza. Aidha Uchakavu wa nyumba za Shirika, Kodi ndogo za nyumba pamoja na Utunzaji mbovu wa nyumba za Serikali kwa wapangaji wanaoishi katika nyumba za Shirika nako kunakwaza maendeleo ya shirika hilo.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyengine tena Kamati inaendelea kuwashauri Shirika kuchukua hatua na mbinu mbadala katika kuhakikisha wale wote wanaodaiwa kulipa kwa kufata utaratibu ili Shirika liweze kuinuka na kutekeleza kazi zake ikiwemo ukarabati wa nyumba.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Ripoti yetu inamalizia kwa kugusia Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Kondomino, Bodi ya Usajili, Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji wa Majengo. Kamati inashauri kufanyiwa kazi kasoro zote zilizoainishwa ili kufikia utekelezaji mzuri na ufanisi wa kazi kwa taasisi hizo.

## WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya tatu inayosimamiwa na Kamati yetu ni Wizara ya Maji, Nishati na Madini, yenye dhamna ya kuhakikisha wananchi wote wanapata maji safi na salama, huduma ya nishati ya umeme na rasilimali zisizorejesheka bila ya usumbufu Mjini na Vijijini. Kamati yetu pamoja na kuthamini juhudi na mipango mizuri na mikubwa ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kila mwananchi, lakini inaendelea na kusikitishwa na changamoto kadhaa zinazokwaza utekelezaji wa Wizara hii katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

### *Hali ya Upatikanaji wa Maji Zanzibar.*

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu imechambua hali halisi ya Upatikanaji wa huduma ya maji hapa Zanzibar ambayo inadaiwa kufikiwa kwa wastani wa asilimia **66%** ya uzalishaji na upatikanaji wa huduma hiyo.

Kamati haikuridhika na takwimu hizo zilizotolewa na ZAWA pamoja na Wizara kwa jumla kutokana na Changamoto kadhaa zinazoikabili sekta ya Maji ikiwemo tatizo la uzalishaji na uvuna wa maji, huku hali ya mivujo na kuchakaa kwa mabomba nazo zikiendelea kukwamisha juhudi za Upatikanaji wa maji hapa nchini. Kamati ina wasiwasi na upatikanaji wa takwimu za upatikanaji wa maji huku ikijiuuliza takwimu hizi zimepatikana vipi, maeneo gani na kwa sampuli gani iliyotumika?

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inalazimika kulitilia mkazo suala hili la tatizo la upatikanaji wa maji, suala ambalo kila mmoja wetu ni shahidi katika majimbo yetu juu yamalalamiko tunayoyapata dhidi ya upatikanaji wa huduma hii muhimu kwa maisha yetu ya kila siku.

Kwa upande mwengine Kamati imebaini kwamba, ZAWA na Idara ya Maendeleo ya Maji kwa ujumla hivi sasa imejikiti zaidi katika usimamizi wa miradi mipya kwa lengo la

kuwapa moyo mkubwa wananchi juu ya upatikanaji wa huduma ya maji huku wakiiacha miradi mikongwe ambayo kwa mtizamo wa Kamati iwapo nayo itaendelezwa inaweza kuchangia kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma ya maji iliyo bora na kwa ufanisi mkubwa.

*Miradi mipya ya ujenzji wa Barabara na Miundombinu ya Maji*

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebani malalamiko ya kisekta juu ya mashirikiano na ushirikishwaji mdogo kati ya watendaji wa ZAWA na Wakandarasi wa Miradi Mipya ya Barabara ambapo Mamlaka hutakiwa kuondosha miundombinu yake bila ya maelekezo ya wapi kwa kuweka miundombinu hiyo jambo ambalo hupelekea usumbufu kwa watendaji.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yangu inazidi kusisitiza haja ya mashirikino na mipango mirefu ya kisekta na kuhakikikisha inazingatia mahitaji ya huduma zote za kijamii hasa katika miradi ya umeme, maji na barabara ili kuepusha uharibifu na usumbufu baina ya taasisi moja na nyengine wakati wa utekelezaji wake.

*Shirika la Umeme Zanzibar ZECO*

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaendelea kusisitiza haja ya kuwepo kwa mashirikiano ya karibu ya kiutendaji miongoni mwa Watendaji wa Shirika hilo ili kuongeza kasi na ufanisi ulliokusudiwa. Kamati inaamini kwamba mashirikiano hayo ndio chachu ya mafanikio ya Shirika hilo na kupunguza malalamiko ndani ya watendaji wenyewe na pia kwa wateja wao.

***Mheshimiwa Spika,*** Hali ya umeme mdogo katika maeneo mengi ambao pia umekua ukikatika katika mara kwa mara katika maeneo mengi ya Zanzibar, nayo ni miongoni mwa changamoto kubwa Kwa ZECO, Kamati inadhani uchakavu wa miundombinu yake, pamoja na kuongezeka kwa kasi idadi ya wateja wapya nako kunachangania changamoto hiyo.

Kamati inashauri Shirika kuzidi kujipanga katika kuboresha upatikanaji wa huduma ya

nishati ya umeme ambapo mahitaji yanaongezeka siku hadi siku. Lakini pia kuwa na mipango ya muda mrefu ambayo itaweza kusaidia kama vile kununua transfoma kubwa zenye kukidhi haja kwa kipindi kisichopungua miaka 15 katika eneo na kuachana na tabia ya kununua transfoma ndogo ambazo baada ya muda mdogo hazikidhi haja na kuleta kero kwa watumiaji wa umeme.

***Mheshimiwa Spika,*** Uwepo wa madeni makubwa kwa Taasisi za SMZ, SMT na Taasisi Binafsi hadi kufikia Shilingi **56,745,448,111.52** nayo ni miongoni mwa Changamoto inayorejesha nyuma utendeji wa shirika hili. Kamati inaisisitiza ZECO kwa kushirikiana na Wizara kuendelea kufatilia wadaiwa wote ili kusawazisha madeni yao na kuliwezesha shirika kutoa huduma bora zaidi.

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)***

***Mheshimiwa Spika***, Ripoti yetu pia imejumuisha uchambuzi katika Mamlaka ua Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati ambapo tumeelezea mapunguzu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa ZURA kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar. Kamati inaishauri ZURA kuhakikisha inaziandikia taasisi za ZAWA na ZECO na kurejesha mrejesho wa yale yote yanayoibuliwa wakati Mamlaka hiyo inapofanya Ukaguzi kwa taasisi inazozisimamia.

***Sekta ya Madini***

***Mheshimiwa Spika,*** imefurahishwa na uamuzi wa Idara ya Nishati na Madini imeanza kupeleka mfumo wa kielektroniki katika ngazi za Wilaya ili kukabili utumiaji wa mfumo wa ***Usimamizi wa Madini*** kwa wananchi, ili kuondoa mrundikano wa maombi ya uvunaji wa rasili mali hiyo. Kamati imebaini kwa sasa mwananchi atapatiwa kibali cha madini ya ujenzi ndani ya masaa nane (8) badala ya siku mbili za hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Eneo la Magari ya Mchanga Taveta, Wilaya ya Magharibi "B" na kulikagua eneo hilo pamoja na kufanya mahojiano na Vijana wanaojishughulisha na biashara ya mchanga katika eneo hilo na kubaini changamoto zifuatazo: -

a) Eneo hilo sio rafiki kiusalama na kimazingira

b) Eneo lipo chini ya Line za Umeme Mkubwa unaotokea Fumba kuelekea Mtoni

c) Shughuli zinazofanyika katika eneo hilo linaikosesha mapato serikali

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inalipatia ufumbuzi suala la magari ya Mchanga Taveta ili kuhakikisha wafanyabiashara hao wanafanya shughuli zao kwa utulivu na usalama na serikali nayo ikiokoa mapato yake.

***Mheshimiwa Spika*,** Kamati pia ilipata fursa ya kukaguwa uhuishwaji wa maeneo ya uvunaji wa rasilimali zisizorejesheka za Wilaya ya Kaskazini B na kushuhudia maeneo kadhaa yanayohuishwa na Serikali yakiwa katika hali isiyoridhisha huko maeneo yanayosimamiwa na watu binafsi yakinawiri vizuri na kuonesha matumaini na dalili njema za kunawiri. Tunaiomba Wizara itafute njia bora na nafuu za uhuishaji wa maeneo yaliyochimbwa kifusi, mawe na mchanga huku ikiweka Sera, Sheria na Kanuni imara za usimamizi wa Madini Zanzibar ili kupata miongozo bora ya kiutendaji katika sekta hiyo.

***Hitimisho***

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inakamilisha Ripoti yake ya Mwaka 2022/2023 kwa kuwapongeza na kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja Viongozi na watendaji wote kwa Ujumla wa Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha kwa umuhimu mkubwa Kamati inakupongeza kwa dhati wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na sekretariati yote ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati

kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha ripoti yake kwa mwaka 2022/2023. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata ili kuweza kufikiwa malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu wa kipekee tunawashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa makatibu wa Kamati yetu ambao ni ndugu **Rahma Kombo Mgeni** na Ndugu **Himid Haji Choko** kwa kuweza kuratibu vyema shughuli za Kamati yetu hadi kufanikisha kupatikana kwa Ripoti hii na hadi hiileo tunaiwasilishwa katika Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho nawaomba waheshimiwa wajumbe kuisoma, kuichangia na hatimae kuikubali ripoti yetu ili hatimae kuongeza uwajibikaji na ufanisi bora na wenye tija katika nchi yetu. Ahsanteni sana kwa kuniskiliza.

***Mheshimiwa Spika*****,** naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.



……………………….

**(Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla),**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**ZANZIBAR.**